



KATIKA SHAURI LA COVENANT BANK FOR WOMEN (TANZANIA) LIMITED, EFATHA BANK LIMITED, NJOMBE COMMUNITY BANK LIMITED, KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LIMITED NA MERU COMMUNITY BANK LIMITED (CHINI YA UFILISI)

NA

KATIKA SHAURI LA SHERIA YA MABENKI NA TAASISI ZA KIFEDHA, 2006 (THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS ACT, 2006)

TAARIFA KWA WENYE AMANA, WADAI NA WADAIWA

Kufuatia BENKI KUU YA TANZANIA kufuta leseni za kufanya biashara ya kibenki za zilizokuwa Covenant Bank for Women (Tanzania) Limited, Efatha Bank Limited, Njombe Community Bank Limited, Kagera Farmers' Co-operative Bank Limited na Meru Community Bank Limited, na kufuatia uteuzi wa BODI YA BIMA YA AMANA (Deposit Insurance Board) kuwa Mfilisi kuanzia tarehe 04 Januari 2018, taarifa inatolewa kwa wenye amana, wadai na wadaiwa kuwa wawe wavumilivu wakati Mfilisi akiandaa utaratibu wa kushughulikia stahiki zao za mujibu wa sheria. Aidha, Mfilisi kwa wakati muafaka atawafahamisha wenye amana, wadai na wadaiwa utaratibu wa malipo wa madai, ulipaji wa madeni na taratibu nyingine zitakazohitajika kwa mujibu wa sheria.

Kwa maelezo ya ziada, tafadhali wasiliana na Mkurugenzi, Bodi ya Bima ya Amana kwa anuani ifuatayo:

2 Mtaa wa Mirambo
Benki Kuu ya Tanzania
Makao Makuu, Ghorofa ya Saba, Mnara wa Kaskazini
S.L.P. 2939
11884, Dar es Salaam
Simu: +255(0)22 2235390
Nukshi: +255(0)22 2234200
Barua Pepe: DIB-INFO@bot.go.tz

BENKI KUU YA TANZANIA

04 Januari 2018